# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Nne – Tarehe 16 Septemba, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kufuta Hasara/Upotevu wa Fedha na Vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia Tarehe 30 Juni, 2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kufuta Hasara/Upotevu wa Fedha na Vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia Tarehe 30 Juni, 2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu!

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa swali letu la kwanza litaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara.

Na. 48

**Mkataba na. 189 wa Kazi za Staha kwa Wafanyakazi wa Majumbani**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaridhia Mkataba Na.189 wa Kazi za Staha kwa Wafanyakazi wa Majumbani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Mkataba huu wa Kimataifa wa kuhusiana na haki za wafanyakazi wa majumbani haujaridhiwa ambapo Serikali inafanya tathmini ya kina kuona kama kuna umhimu wa kuridhia na kuwa masuala mengi yaliyoko katika Mkataba huu yanatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019. Aidha, siyo kila Mkataba wa Kimataifa unaridhiwa. Tunaridhia mikataba ya msingi *(Core Conventions)* ambapo kwa Mikataba isiyo ya lazima *(Other Conventions)* uridhiaji wake utazingatia mila, desturi na hali ya uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kushauriana na wadau katika suala hili. Nitumie fursa hii kuwaomba wadau kuendelea kutoa maoni ya njia bora ya kuendelea kuboresha maslahi na haki za wafanyakazi wa majumbani kwa kuzingatia mila, desturi na hali ya nchi yetu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwanini Serikali isiridhie sehemu ya mkataba huo ambayo haina matatizo wala ukakasi ili kuwasaidia wafanyakazi wa majumbani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Serikali inawasaidaje wafanyakazi wa *private sectors* wakiwemo wa mahoteli na kwenye baa waweze kujiunga na vyama vya wafanyakazi ili kulinda maslahi yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mambo ambayo hayana madhara yanayoendana na mila, tamaduni na desturi ya nchi yetu, tayari sheria yetu ya ajira na mahusiano kazini ya sura namba 366 imeshayazingatia hayo na tumeyafanyia *domestication* kwa maana ya kuchukua na kuyaweka kwenye sheria zetu za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika eneo hilo, siyo mikataba yote ya Kimataifa ambayo tunairidhia kwa ujumla wake. Tuna haki kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa ya kusaini tu, lakini kuna *process* nyingine ya kufanya *ratification* na baada ya hapo unaweza ukawa unafanya *reservation*. Kwa hiyo, tuna *reservation* kwenye baadhi ya vifungu vya Mkataba huu wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo, nimhakikishie Mheshimiwa tayari Serikali ina utaratibu mzuri wa kuhusiana na Mikataba ya Kimataifa kwenye masuala ya haki za wafanyakazi kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani *(International Labour Organization)*. Sambamba na hilo, tunaendelea kuratibu hata wale wafanyakazi wa majumbani walio nje nchi, kwa mfano, kwa nchi za Mashariki ya Kati, kule Oman, wako zaidi ya wafanyakazi

14,000 ambao walikuwa wanafanya kazi kule na 55 wako kwenye kada nyingine tofauti na ufanyakazi wa majumbani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, umejibu vizuri hilo swali, tuendelee.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili la kuhusiana na wafanyakazi wa hotelini kuingia kwenye vyama vya wafanyakazi, tunayo pia sheria inayohusiana na masuala ya *Trade Unions* ambayo ni sheria inayoratibu uwepo wa *Trade Unions.* Vyama hivi vya wafanyakazi wana haki ya kukusanya wanachama katika maeneo mbalimbali yaliyosajiliwa. Kwa hiyo, tayari utaratibu huo unafanyika na tumeshaanza kutembelea baadhi ya hoteli na maeneo mengine kuhakikisha wafanyakazi hawa wanapewa mikataba na kulinda haki zao za msingi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

Na. 49

**Fedha za Ujenzi wa Kituo cha Afya Lyamungungwe na Kihanga – Kalenga**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kujenga Vituo vya Afya katika Kata ya Lyamugungwe na Kihanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais,TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilipeleka Shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vitatu katika Wilaya ya Iringa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kupitia mapato ya ndani imetenga Shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Magulilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Kata ya Lyamungungwe na Kihanga, Serikali itajenga Kituo cha Afya cha kimkakati katika Kata ya Kihanga ambayo itatengewa fedha kwenye bajeti ya mwaka 2024/2025. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini mpango wake wa 2024/2025 ni mbali sana. Ione uwezekano wa kurudisha kati 2023/2024. Maswali mawili ya nyongeza ni haya:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Mgama, kipo kituo cha afya na wananchi walishajenga msingi wa wodi, sasa uwezo wao wa kuendelea kujenga ni mdogo: Je, ni lini Serikali itatusaidia kuleta fedha ili tujenge wodi ili wananchi wa vijiji 12 wanaohudumiwa hapo wapate huduma?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Pamoja na kwamba umesema Halmashauri itatenga Shilingi milioni 400, uwezo wa Halmashauri yetu bado siyo mkubwa hivyo. Aliyetangulia, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, aliahidi kuleta Shilingi milioni 300. Ni lini fedha hizo zitakuja Magulilwa ili tukamilishe hiki kituo cha afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Kata ya Mgama kwa kutoa nguvu zao kujenga kituo cha afya na kujenga msingi kwa ajili ya wodi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumemwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini, afanye tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya ukamilishaji wa wodi hiyo ili Serikali ione namna ya kutafuta fedha kwa kushirikiana Halmashauri kwa maana ya mapato ya ndani kukamilisha ujenzi wa wodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, aliahidi kupeleka Shilingi milioni 300 fedha ya Serikali kwa ajili ya kujenga kituo cha afya pale Magulilwa. Katika jibu la msingi tumetenga Shilingi milioni 400 kupitia mapato ambayo ndiyo fedha ya Serikali hiyo hiyo kwa kwa jili ya ujenzi wa kituo cha afya hicho. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kule Magu Lutale, Wamanga na Igogo, kuna uhitaji mkubwa sana wa vituo vya afya: Je, Serikali ina mpango gani kuyaangalia maeneo yale ambayo yako mbali na huduma? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Magu, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge ikiwepo ya Mtalia na hizo nyingine mbili kwa kadri ya uhitaji wa vituo vya afya, Serikali ilishatoa maelekezo kwamba Halmashauri ziainishe kata za kimkakati kwa ajili ya kujenga vituo vya afya, kwa kuwa hatujengi kituo cha afya kila kata wala hatujengi zahanati kila Kijiji, bali tunajenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati ambazo zina vigezo ambavyo vinaelezea na pia zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba twende tukaainishe haya maeneo kama ni maeneo ya kimkakati na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Magu alete Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kwenda hatua inayofuata.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, Kata ya Korongwe na Kata ya Mkwamba kuna umbali wa kutosha kufika katika hospitali ya wilaya, na hizo kata zote mbili hazina vituo vya afya: Nataka kujua mkakati wa Serikali ili kuwaokoa wanawake ambao wamekuwa wanajifungulia njiani na kupewa *penalty,* wanalipa Shilingi 50,000?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Nkasi ni miongoni mwa Halmashauri ambazo bado zina kata ambazo hazina vituo vya afya, na tayari Mkurugenzi alishawasilisha kata za kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kata hizi mbili ni sehemu ya kata ambazo tutakwenda kutafuta fedha, kwa kushirikiana na Halmashauri, kwa maana ya mapato ya ndani na Serikali Kuu ili kuanza ujenzi wa vituo vya afya hivi kwa awamu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Komanya.

Na. 50

**Kukamilisha Maboma ya Zahanati – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, ni lini Maboma ya Zahanati Vijiji vya Lata, Ikigijo, Lukale, Malwilo, Bulyanaga, Shushuni, Nata, Usiulize na Igushilu yatakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilipeleka Shilingi milioni 200 katika Wilaya ya Meatu kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati nne. Aidha, katika mwaka 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi milioni 200 kutoka Serikali Kuu na Shilingi milioni 100 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati za Mwandukisesa, Masanga, Mwanyahina, Mwabagashi na Ikigijo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 kiasi cha Shilingi milioni 100 kitatengwa kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati za Igushilu na Nata. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Msingi wa uanzishwaji wa maboma ya zahanati ulitokana na uliokuwa mradi wa uendelezaji wa mitaji katika Serikali za Mitaa. Hivyo katika Bunge la Kumi na Moja, lilitaka Serikali kukamilisha maboma hayo baada ya mradi huo kwisha.

**NAIBU SPIKA:** Swali, swali, Mheshimiwa Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni haja ya kupeleka mwongozo wa matumizi ya fedha katika fedha za kukamilisha maboma ya zahanati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takribani ni miaka miwili sasa Serikali imepeleka fedha 2021/2022: Je, Serikali iko tayari kufanya sensa ya kuangalia fedha zilizopelekwa kukamilisha maboma, zinaendana na maboma yaliyokamilishwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipeleka mwongozo wa namna ambavyo fedha zinazopelekwa kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati Shilingi milioni 50 kwa kila boma zinatakiwa kutumika na kukamilisha maboma yale. Moja ya maelekezo ilikuwa ni kwamba, boma ambalo linaombewa fedha, Shilingi milioni 50 lazima liwe limefika hatua ya *renter*, siyo msingi au chini ya *renter*. Hesabu zilifanywa kwamba Shilingi milioni 50 ipelekwe kwenye jengo ambalo limefikia hatua ya *renter* linakamilika na kuanza kutoa huduma za afya mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kila inapopeleka fedha, inapeleka na mwongozo, na pia tunafuatilia kuona utekelezaji wa miradi hiyo kwa mujibu wa mwongozo uliopelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na kufanya tathmini kama fedha ambazo zilipelekwa kwa ujenzi wa maboma zimekamilisha; katika mwaka wa fedha uliopita zaidi ya maboma 555 yamelekewa Shilingi milioni 50, lakini zaidi ya asilimia 85 mpaka Juni mwaka huu yalikuwa yamekamilika, na yako hatua za mwisho za kusajiliwa. Tunaendelea kufanya tathmini kuhakikisha fedha hizo zinaleta tija kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu. Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Mbugani katika Jimbo la Tabora Mjini ina uhitaji mkubwa sana wa zahanati. Sijui Serikali ina mpango gani wa kuisaidia Kata hiyo ya Mbugani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hii ya Mbugani ambayo ina uhitaji wa zahanati, nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, kufanya tathmini kujiridhisha na vigezo vya kujenga zahanati ya kimkakati na baada ya hapo kuona mapato ya ndani, na pia kuleta maombi Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kwa kutumia mapato ya ndani na Serikali kuu tuone uwezekano wa kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Anton Albert Mwantona.

No. 51

**Majengo Yaliyokuwa ya Zahanati ya Ukoma Kuwa Kituo cha Afya**

**MHE ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati majengo ya Zahanati ya Ukoma kuwa Kituo cha Afya cha Kata ya Kisondela Wilayani Rungwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Jimbo la Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Majengo ya Zahanati ya Makete, Ukoma yaliyokuwa yakitumika kwa wagonjwa wa ukoma ni chakavu. Aidha, kwa kuwa eneo la Kata hii halikidhi vigezo vya kuwa na Kituo cha Afya cha Kimkakati kwa kuzingatia idadi ya watu wasiofikia angalau 10,000, Serikali itaendelea kuitumia zahanati inayotumia moja ya majengo haya kutoa huduma kwa wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kata hiyo itakapokidhi vigezo vya kuwa na Kituo cha Afya cha kimkakati, Serikali itafanya maamuzi stahiki. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantona.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwamba imetujengea vituo vitatu vya afya kwa mwaka uliopita, ambapo kuna Kituo cha Ndanto, Kituo cha Kiimo pamoja na Kituo cha Ikinjola ambavyo viko mwishoni kabisa kukamilika na watumishi wameshapelekwa; je, ni lini vifaa tiba katika vituo hivyo vya afya vitapelekwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye Kituo cha Afya cha Masukuru, jengo la *X-Ra,* liko tayari, pia na jengo la *mortuary* liko tayari, lakini kwa bahati mbaya sana *x-ray* hatuna na mtumishi wa *mortuary* pale katika Kituo cha Afya Masukuru hakuna. Ni lini *x-ray* pamoja na mtumishi wa *mortuary* katika Kituo cha Afya cha Masukuru watapelekwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Jimbo la Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipokee shukrani za Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali hii Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kujenga Vituo vya Afya vitatu ndani ya mwaka mmoja. Nimhakikishie kwamba mipango ya ujenzi wa Vituo vya Afya inakwenda sambamba na mipango ya ununuzi wa vifaa tiba. Katika bajeti ya mwaka huu Serikali imetenga jumla

shilingi bilioni 69.95 kwa ajili ya vifaa tiba kwenye vituo vya afya 530. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia tutatoa kipaumbele kwenye vituo vya afya ambavyo vimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na ukosefu wa mashine ya *x-ray* na mtumishi wa *mortuary*, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kununua vifaa tiba hivi kwa awamu. Kwa hiyo, mara pale tutakaponunua *x-ray* za kutosha basi kituo hiki cha afya pia kitatazamwa pamoja na kupelekewa mtumishi wa *mortuary*, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau, halafu Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Katika Kata ya Wazo, Jimbo la Kawe tayari zahanati imekamilika, lakini hakuna Jengo la Mama na Mtoto. Ni lini Serikali itajenga jengo hilo ili kunusuru uhai wa akinamama hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika Kata ya Wazo zahanati imekwishajengwa lakini hakuna Jengo la Mama na Mtoto, lakini nafahamu Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni haiwezi kushindwa kujenga Jengo la Mama na Mtoto. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kutenga fedha kwa ajili ya kujenga Jengo la Mama na Mtoto katika zahanati hii kwenye Kata ya Wazo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spikaa, nakushukuru sana. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imeshafanya tathmini kuhusu mahitaji ya maeneo ya kujenga vituo vya afya ambako kuna watu wengi na ni mbali. Kituo cha Afya katika eneo la Kata za Igigwa, Kiloleli, Ipole na Usunga. Je, ni lini Serikali itatusaidia kujenga vituo hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda, Mbunge wa Jimbo la Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kuainisha maeneo yote ambayo ni ya kimkakati kwa ajili ya kujenga Vituo vya Afya kwenye Kata na Tarafa za kimkakati na nakumbuka Mheshimiwa Mbunge alikwisha wasilisha kata hizo kwa ajili ya kujenga hivyo vituo vya afya na sisi tunafanya tathmini kujiridhisha tu na vigezo vile, lakini nimhakikishie kwamba tunafahamu Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ni moja ya halmashauri kubwa na ina umbali mkubwa kati ya kata na kata, hivyo tutaweka kipaumbele katika ujenzi wa vituo hivyo vya afya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Kuchauka.

No. 52

**Kufanya Mapitio ya Upimaji wa Ardhi wa Mwaka 1970**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kufanya mapitio ya upimaji wa vijiji nchini kwa kuwa migogoro mingi imesababishwa na upimaji usio shirikishi wa mwaka 1970?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kabla ya kujibu swali lake la msingi kuwa kilichofanyika katika miaka ya 1970 haikuwa upimaji wa vijiji bali ilikuwa ni Operesheni Maalum ya Serikali ya kuanzisha Vijiji vya Ujamaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya 2000 Serikali ilitekeleza *Programu* ya upimaji wa vijiji kwa lengo la kuvifanya vijiji kuwa mamlaka kamili za usimamzi wa ardhi za vijiji. Mathalani, katika Mkoa wa Lindi jumla ya vijijii 401 kati ya vijiji 523 vikiwemo Vijiji vya Wilaya ya Liwale vilipimwa kwa njia shirikishi na kuwekewa alama za mipaka.

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kweli vijiji hivi kama majibu ya msingi yanavyosema; ni kweli upimaji huu ulifanywa lakini walio wengi wanaolalamika ni kwamba upimaji haukuwa shirikishi. Kwa mfano, kuna mgogoro wa Mkutano na Kikunyungu, Kipelele, Nangumbu au Ngongowele na Ngunja. Wanachozungumza pale ni kwamba yale mawe wakati wanabeba kuna mahali walichoka wakayatunza mahali. Matokeo yake hawakurudi pale, kwa hiyo, yule aliyekuja kuchukua a-*coordinate* majira ya nukta akachukulia pale. Kwa hiyo, hicho ndiyo chanzo cha migogo mingi kwenye hivi vijiji ambavyo nimevitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mgogoro kati ya Wilaya ya Kilwa na Wilaya ya Liwale kwenye Vijiji vya Nanjilinji na Milui. Mgogoro wake *scenario* yake inafanana na hiyo hiyo, kwamba wakati wanapima wakazi wa wilaya hizi mbili zote hawakushirikishwa. Sasa Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kufuatana nami baada ya Bunge hili twende Liwale akatatue migogoro hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya changamoto iliyotokea ni kweli yako baadhi ya maeneo ambayo yana changamoto hizo. Nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge tutapanga ziara twende tukakutane na wananchi wake ili kumaliza kero katika maeneo yake. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mheshimiwa Shekilindi. Mheshimiwa Shekilindi, tafuta *microphone* inayofanya kazi. Madawa yamezidi kwenye meza hapo. (*Kicheko)*

Na. 53

**Ujenzi wa Uwanja wa Michezo - Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Uwanja wa Michezo katika Mji wa Lushoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Taifa ya mwaka 1995 ibara ya 7(i) – (vii), jukumu la ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya michezo ni jukumu la Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na Wadau wa Sekta ya Michezo zikiwemo Taasisi, Mashirika na Watu Binafsi. Hivyo, napenda kuzikumbusha na kuzielekeza halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Lushoto kuzingatia matakwa ya Sera ya Michezo kwa kutenga fedha kutoka katika mapato ya ndani kwa ajili ya kujenga na kukarabati miundombinu ya michezo kwenye maeneo yao. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Lushoto kuna uwanja wa muda mrefu sana lakini uwanja ule unatakiwa ukarabati. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba inapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati uwanja ule?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa michezo ni ajira. Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kuibua, kubaini na kuwahakiki vijana ambao wanataaluma ya michezo hususan Wilaya ya Lushoto hasa Lushoto Vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shekilindi swali lake la kwanza amependa kufahamu ni lini Serikali inatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja huo wa Lushoto lakini viwanja vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majibu yangu ya msingi nimeeleza kwamba Sera yetu ya michezo imezitaka Serikali kwa ngazi zote Serikali Kuu lakini Serikali za Mitaa kutenga fedha. Ni rahisi sana kama halmashauri zetu, Wakurugenzi pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani tukasimamia kupitia Idara ya Michezo fedha zikatengwa na viwanja hivi vitajengwa na ninyi ni mashahidi tumeanza sisi kwenye wizara bajeti iliyopita tumetenga zaidi ya bilioni 10 kwa ajili ya kujenga viwanja vya kitaifa. Kwa hiyo, naomba nitoe rai tuendelee kutenga fedha kwa Serikali kwa ngazi zote ili tujenge viwanja hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Mheshimiwa Shekilindi amependa kufahamu ni jinsi gani tunashirikiana na TAMISEMI pia kuhakikisha vipaji vinaibuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wizara tumeshatoa maelekezo kwa ngazi zote na kwa vyama vyetu na mashirikisho, kwamba vipaji vinapoibuliwa vyama na mashirikisho yaweze kushiriki. Naomba nipongeze kwa niaba ya Waziri, Wabunge na Madiwani ambao wamekuwa wakichezesha ligi mbalimbali katika maeneo yao, maana yake wanaibua vipaji. Sisi kama Wizara tunakuja na mtaa kwa mtaa kuhakikisha kwamba tunapofika kwenye lengo la Taifa la Taifa cup tunahakikisha kwamba huko chini vipaji vimeibuliwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; kwanza nimpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Pauline Gekul kwa kujibu maswali vizuri. Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunashirikiana vema na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo imetuelekeza kupitia Sanaa, Michezo na Utamaduni tunatengeneza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Shule za Msingi na Sekondari kote nchini kuhakikisha maeneo yanapimwa na tunapata haTi kufika Disemba, 30; na nimeelekeza kopi ya hati ije Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili niweze kujiridhisha kila shule ya msingi na sekondari imepimwa na kupata hati. Tunafanya hivi ili kuhakikisha maeneo ya shule tunapunguza uvamizi ikiwemo maeneo ya michezo kwa maana ya viwanja vya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie nafasi hii kuwaagiza Wakurugenzi kufanya kipaumbele kwenye bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kutenga fedha kwa ajili ya kujenga viwanja vya michezo ni moja ya vipaumbele katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Serikali ina mpango gani kujenga uwanja wa michezo Mkoa wa Simiyu unaoendana na hadhi ya Mkoa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi. Naomba nijibu swali la Mheshimiwa Midimu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mikoa yetu tuna ma-*RAS* ambao ni wenyeviti wa michezo, lakini kwenye wilaya zetu tuna ma-*DAS* ambao ni wenyeviti wa michezo, lakini tuna Wakurugenzi wetu tuna Maafisa Michezo kama ambavyo nimejibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba ni jukumu sasa Serikali za Mitaa wakatenga bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo linapaswa lianze haraka ili wananchi ambao wana vipaji vyao viendelee kuibuliwa kwa kucheza katika viwanja ambavyo ni vizuri. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Mkoa wa Simiyu kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali haijawekeza sana kwenye viwanja vya masumbwi na kupelekea wanandondi kufanya mazoezi kwa kutumia njia za asili ikiwemo matairi. Je, ni lini

Serikali itawekeza kujenga maeneo sahihi ambayo wanamasumbwi hao waweze kufanikiwa kama kijana wetu Mwakinyo anavyofanya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mwakagenda pamoja na Wabunge wengine wote kuhakikisha kwamba mchezo huu wa ngumi unafika mbali. Nimhakikishie kwamba, miongoni mwa maelekezo ambayo tunatoa katika nyanja mbalimbali na katika mashirikisho ni kuhakikisha kwamba miundombinu inajengwa, kwa sababu kila chama cha mchezo kina jukumu kwa mujibu wa sera yetu kuhakikisha vijanja na miundombinu inajengwa. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kusimamia kama wizara kuhakikisha kwamba hayo maeneo yanapatikana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mtu usijione una mwili mkubwa ukajiona ni *boxer* mzuri.

Mheshimiwa Naibu Waziri nakupongeza sana, kwa kweli wizara yenu toka umeanza wewe, Waziri wako, Makatibu Wakuu wawili mmeleta uhai mkubwa sana kwenye Wizara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Tabasamu Mwagao.

Na. 54

**Ujenzi wa Banda la Ukaguzi wa Samaki Chifunfu**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa banda la ukaguzi na kupokea samaki wabichi katika Kata ya Chifunfu utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa banda la kupokelea samaki Chifunfu uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ulianza mwezi Mei, 2021 chini ya Mkandarasi *M/S Fast Construction Company Limited* ya Mkoani Mwanza kwa thamani ya shilingi 124,592,064.00 ambapo hadi sasa ujenzi umefikia hatua ya kuezeka na Mkandarasi ameshalipwa kiasi cha shilingi 95,768,193.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya ujenzi wa banda hilo ilipangwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi sita, hata hivyo Mkandarasi hakuweza kukamilisha kazi hiyo kwa mujibu wa mkataba, hivyo Serikali imechukua hatua za kusitisha Mkataba wa Mkandarasi huyo na hatua zingine za kisheria zinaendelea dhidi yake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam. *(Kicheko)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mkandarasi huyu alipewa kazi hii toka mwaka jana Mei, 2021 na kazi yenye ilikuwa ni sehemu ya kutengeneza mwalo wa kupokelea samaki pamoja na vipimo vya samaki, hauoni sasa muda tayari umeshafika zaidi ya mwaka mmoja na miezi minne, ni lini sasa kazi hiyo ya ujenzi wa banda hilo utakamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza ni kwamba, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika katika eneo hilo la mradi na pamoja na kutembelea eneo hilo alikwenda pia kuangalia mabwawa ya kunyweshea mifugo katika Jimbo la Sengerema, lakini mpaka leo hii mabwawa hayo hayajapata fedha. Je, ni lini fedha zitaletwa kwa ajili ya kuyaziba mabwawa tisa yaliyopasuka katika Jimbo la Sengerema?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Tabasamu, Mbunge wa Sengerema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kukamilisha unafanyika kwa haraka mara baada ya kuvunja mkataba, hivi sasa wataalam wetu wapo kazini kuhakikisha kwamba kazi ile ya wananchi inakamilika ili waweze kupata huduma wanayostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili anataka kujua juu ya mabwawa yake lini yatapata fedha. Tayari kwa utaratibu wa Sheria ya Manunuzi tumekwishatangaza tenda na tupo katika hatua ya kupata wakandarasi na hatimaye yale yaliyopangiwa kwenye jimbo lake yatapata fedha na wakandarasi watatekeleza kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Tabasabu kwa ushirikiano mkubwa anaotupatia, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Pareso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Hapa siku za karibuni tumesikia taarifa kupitia vyombo vya habari kwamba uhifadhi wa samaki hapa nchini kwenye baadhi ya maeneo, samaki wanahifadhiwa kwa kutumia dawa za kuhifadhia maiti, jambo ambalo linaleta taharuki kwa wananchi na wananchi hawajui nini cha kufanya ili wasipate hao samaki waliohifadhiwa kwa namna hiyo.

Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha samaki hao hawahifadhiwi kwa vitu hivyo ambavyo vinasababisha kansa kwa Watanzania? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Swali la Msingi ni kwa ujenzi wa banda lakini kwa vile swali ni muhimu, Mheshimiwa Waziri jibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili alilolisema Mheshimiwa Paresso ni *hypothesis* halina hakika hadi sasa hivi. Ni kwamba watu wanahisia kuwa kiko kitu cha namna hiyo na ndiyo maana Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuwa Jijini Mwanza aliagiza Wizara ya Afya ifanye utafiti ili kama ni kweli kinafanyika kitu cha namna hiyo basi kizuiwe mara moja. Naomba niwatoe hofu Watanzania hakuna jambo linalohusu tuchukue samaki kutoka Mwanza tulete Dodoma au tupeleke Dar es Salaam kwa kuhifadhi na maji ya maiti, halipo jambo la namna hiyo! Naomba wawe na uhakika ya kwamba samaki wanaovuliwa na

wavuvi wetu na wanaokwenda katika masoko mbalimbali wako salama hawana shaka yoyote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Getere.

Na. 55

**Fursa anazopata askari anayeoa au kuolewa na askari mwenzake**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, ni fursa zipi anazopata Askari anayeoa au kuolewa na Askari mwenzake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni, miongozo na taratibu za Majeshi ya Ulinzi, kila Afisa na Askari hupewa stahiki kulingana na cheo chake. Endapo Afisa au Askari ataoa au kuolewa na mwenzake, haitaathiri stahiki zake. Aidha, hakuna fursa za kipekee anazopata Afisa au Askari aliyeoa au kuolewa na mwenzake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka mingi sasa toka ukoloni vijana wetu wanaoajiriwa na Jeshi la Kujenga Taifa wanapewa miaka Sita kabla ya kuolewa au kuoa. Kwa kuwa, magonjwa yamekuwa mengi na kwa kuwa *stress* za Askari wetu zimekuwa nyingi.

Je, ni lini Serikali itapunguza muda huu wa miaka Sita kuwa miaka Mitatu au Miwil?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni muda sasa tunapeleka vijana wetu JKT tunapeleka vijana 2,000 au 1,000 wanachukuliwa labda 50 wanaajiriwa wengine wanarudi nyumbani. Je, ni lini sasa Serikali itakuja na mpango mkakati wa kuandaa vijana wanaorudi nyumbani kuwapa ufundi wa kutosha na saikolojia ili wasiwe panya *road*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Getere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kumpongeza kwa kuwa mdau wa karibu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kuwatetea wapiganaji wetu. Swali lake la kwanza ambalo ni kuhusu umri, napenda kwanza nitoe ufafanuzi kwamba ni kweli kwamba Maafisa na Maaskari wenye elimu ya darasa la saba hadi kidato cha sita na wenye Stashahada wao ndiyo hukaa miaka Sita kabla ya kuolewa. Yapo makundi mengine kama wenye shahada ya kwanza wao hukaa kama makapera kwa miaka Minne na wenye Shahada ya Uzamili, wao hukaa kwa miaka mitatu na wenye Shahada ya Uzamivu wenyewe hawana muda wa kukaa kwenye ukapera na hii ni kutokana na aina ya majukumu ambayo maaskari hawa wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Askari ambao nimewataja katika kundi la kwanza hao huwa ni vijana wadodo wanajiunga wakiwa na umri wa miaka 18 na kuendelea, kwa hiyo huhitaji kwanza kukomaa. Majukumu ya Jeshi ni majukumu mahususi lakini pia hawa ndiyo wanategemewa kama wapiganaji kwa hiyo huendelea na kozi mbalimbali na kuhakikisha kwamba wako imara wakati wote. Kwa hiyo, miaka hii Sita iliyowekwa imewekwa baada ya kufanya uchunguzi lakini pia kuzingatia vigezo mbalimbali. Kwa hiyo, kama tunaweza kubadilisha sidhani kama hilo linawezekana kwa sasa kwa sababu utafiti ulifanyika na lazima iwe hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii pia inatokana na aina ya majukumu ambayo wanafanya. Wengine wanapoajiriwa kama Madaktari huenda moja kwa moja kufanya hiyo kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umeeleweka umejibu vizuri sana tuende swali la pili.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Swali la pili ambalo linahusiana na vijana wanaokwenda JKT kwamba ni wengi lakini wanaoajiriwa ni wachache. Kwanza ninapenda kueleza kwamba madhumuni ya vijana kujiunga na JKT ni kuwajengea uzalendo, kuwajengea ukakamamu lakini kuwapa stadi mbalimbali ili baada ya hapo waende kujiajiri. Madhumuni siyo kutoa ajira kwa vijana hawa, hilo linafanyika vijana hawa wanafundishwa stadi mbalimbali ili baada ya hapo waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tuna mpango gani, ni kweli nasi tumeona kwamba pamoja na kuwapa stadi mbalimbali bado kuna umuhimu kuwawezesha vijana hawa kujitegemea. Kwa hiyo, tumeanza kufanya kazi hii na tayari katika mpango wa *block farming* kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, tutaona jinsi gani tutaweza kuchukua baadhi ya vijana, lakini bado tunaendelea kulichakata suala hili tuweze kuja na *program* nzuri zaidi ambazo zitawawezesha vijana hawa kujiajiri baada ya kupata stadi ambazo tunawapatia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri tunaendelea Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Kanyasu.

Na. 56

**Kiwanda cha Kasamwa Kusimamisha Uzalishaji**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza:-

Je, ni zipi sababu za Kiwanda cha Pamba na Mafuta cha Kasamwa kusimamisha uzalishaji kwa muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Viwanda na Biashara. Ameshauliza swali.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Pamba na Mafuta cha Kasamwa kilisitisha shughuli za uzalishaji mwaka 2012 kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo teknolojia iliyopitwa na wakati, ukosefu wa vipuri, gharama kubwa za uendeshaji hususani maji na umeme, uhitaji wa idadi kubwa ya wafanyakazi na ukosefu wa malighafi. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kwamba baadhi ya viwanda vitafufuliwa kwa ubia wa ushirika na mifuko ya jamii. Sasa ninataka kujua ahadi hiyo imefikia wapi.

MheshimiwaNaibu Spika, swali langu la pili, hivi karibuni nchi yetu ilikumbwa na uhaba mkubwa wa mafuta ya kupikia. Malighafi ya mafuta ya kupikia ni pamba ambayo ipo nyingi kwenye eneo hilo.

Je, ni mkakati gani sasa ambao Serikali inao kuhakikisha kwamba kiwanda hicho kinafanya kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Constantine Kanyasu Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kweli, ni jitihada ya Serikali kuona viwanda vyetu vinafanya kazi/vinafufuliwa moja ya kimkakati ilikuwa ni kuhusisha mifuko yetu ya jamii kuona nayo inashiriki katika kuzalisha au kufufua kiwanda hiki cha Kasamwa, lakini kutokana na stadi iliyofanywa na wenzetu wa *NSSF* ilionekana kwamba wakati ule bado haina tija kwa wao kuwekeza kulingana na malengo ya mifuko hii ya jamiii. Kwa hiyo, hilo bado linafanyiwa kazi kuona kama kutakuwa na tija ili kuwekeza katika kiwanda hiki cha Kasamwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili mkakati wa Serikali ni kweli, moja ya maeneo ambayo Serikali imeweka mkazo ni kwenye sekta ya kilimo kuona tunaboresha kilimo ili tuwe na malighafi muhimu kwa ajili ya kuzalisha mafuta ya kula, mojawapo ni mafuta ambayo yanatokana na zao la pamba kwa maana ya mbegu za pamba. Kwa hiyo, uzalishaji utaongezeka na hivyo tunaamini viwanda hivi moja ya changamoto ilikuwa ni malighafi kwa hiyo vitakwenda kupata malighafi, ambayo itatumika pia kuzalisha pamoja na bidhaa nyingine na mafuta ya kula ambayo yanatokana na mbegu za pamba. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa unaitwa nani?

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naitwa Mwakamo.

**NAIBU SPIKA:** Haya karibu.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Pwani unaongoza kwa zao kubwa la korosho. Je, nini mkakati wa Serikali kufufua Kiwanda cha Korosho TANITA Kibaha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo pia tunalenga katika kuhakikisha tunaongeza thamani ni kwenye zao la korosho. Viwanda vingi ambavyo vilikuwa havifanyi kazi, mkakati wa kwanza ni kuona vile inavyowezekana kurudisha katika mikono ya Serikali ili tutafutie wawekezaji wengine lakini pia pili, ni kuvutia wawekezaji wapya kuwekeza katika viwanda vipya ambavyo navyo vitaongeza kazi ya kuchakata zao la korosho ili kuziongezea

thamani katika Mikoa ya Pwani na Mikoa ya Nyanda za Kusini ambao wanalima zaidi zao la Korosho. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Madini. Mheshimiwa Aloyce John Kamamba.

Na. 57

**Kupatikana kwa Madini Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza: -

Je, Serikali ina taarifa juu ya madini yanayopatikana Kakonko na wananchi wananufaikaje nayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania *(Geological Survey of Tanzania - GST),* Wilaya ya Kakonko ina madini yafuatayo; dhahabu katika Kata za Nyamtukuza, Gwanumpu, Muhange na Kasuga. Pia ina madini ya vito aina ya Agate katika Kata za Gwanumpu na Kasanda na ina madini ya ujenzi katika Kata zote za Wilaya ya Kakonko.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imetoa leseni 27 za wachimbaji wadogo wa madini katika maeneo tofauti ya Kakonko kama ifuatavyo:- Dhahabu leseni 21, mawe ya chokaa leseni Mbili, shaba leseni Moja, kokoto leseni Tatu, mchanga leseni Moja, chuma leseni Moja na mawe leseni Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uwepo wa leseni za uchimbaji mdogo wa madini ambapo migodi huhitaji watu wengi wa kuzalisha, hivyo kwa njia hiyo wananchi wananufaika na ajira za moja kwa moja katika migodi kwa kutoa huduma mbalimbali kama chakula, malazi, usafirishaji na kadhalika, hivyo kuongeza manufaa ya kiuchumi kwa wananchi wa Wilaya husika na hususani kwa Wilaya ya Kakonko. Ahsante sana.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamamba.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Aidha, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa madini hayo katika Wilaya yetu ya Kakonko ni uthibitisho wa utajiri na hazina kubwa ya madini katika Wilaya yetu.

Je, ni lini sasa Serikali itaanza uchimbaji mkubwa ili wananchi na Serikali iweze kufaidi kwa kiwango kikubwa zaidi? *(Makofi)*

Swali la pili, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwawezesha wananchi na wachimbaji wadogo wadogo mtaji ili uchimbaji uweze kufanyika kwa tija? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce John Kamamba Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa lini uchimbaji mkubwa utafanyika katika maeneo yenye madini Wilayani kwake, napenda kumjulisha kwamba Taasisi yetu ya Utafiti wa Kijiolojia na Madini *(GST)* wanaendelea na utafiti katika maeneo mbalimbali nchini na pale wanapobaini kiwango cha madini yanayopatikana katika eneo husika wanaendelea kutangaza fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wakubwa wenye mitaji mikubwa, ambao kimsingi wakija wanaingia katika ubia na wachimbaji wadogo walioko katika maeneo yale.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umeshajibu vizuri endelea na swali lake la pili.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili Wizara ya Madini tumeshaingia makubaliano na taasisi za kifedha za ndani ikiwepo Benki ya *KCB*, *NMB*, *NBC*, *CRDB* ya kuwapa wachimbaji wadogo mitaji waliokidhi vigezo ili waweze kuchimba madini hayo kwa tija. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nicodemas.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kumuuliza Waziri Wilaya ya Mbogwe ina migodi midogo midogo inayomilikiwa na wachimbaji wadogo.

Je, Wizara imejipangaje kuwanufaisha wachimbaji hao wadogo ili kusudi na wao waone matunda kwenye Serikali yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika nchi yetu tuna wachimbaji wadogo katika sehemu mbalimbali, wenye leseni na moja ya kazi kubwa ya Wizara kupitia Taasisi zake za *STAMICO* na *GST* ni kuwajengea uwezo kwa kuwapa elimu juu ya Sheria ya Madini, Kanuni za Madini na namna ya uchimbaji bora pamoja na kuwatafutia fursa kwa wawekezaji wakubwa wanaokuja kutafuta madini katika maeneo ambayo yameshafanyiwa utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuishii hapo wachimbaji wadogo hawa pia tunaendelea kuwapelekea elimu ya kujiunga na kujisajili, waweze kufanya uchimbaji wenye tija kupitia taarifa za kijiolojia zinazoonesha madini yanayopatikana katika maeneo yao huko.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Katimba.

Na. 58

**Utaratibu wa Biashara Mpya kutakiwa Kulipa Kodi ya Mapato kabla ya Biashara kuanza**

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaondoa utaratibu wa biashara mpya kutakiwa kulipa kodi ya mapato kabla ya biashara kuanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2019/2020, Serikali ilifuta utaratibu kwa walipakodi kulipa kodi kabla ya kuanza biashara. Kufuatia mabadiliko hayo, walipakodi wote wanatakiwa kulipa kodi miezi Sita (6) baada ya kufungua biashara, ili kutoa nafasi ya kujiimarisha kibiashara. Aidha, utozaji wa kodi ya mapato hufanyika kulingana na mapato yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka husika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kama Serikali ilivyosema kwamba imetoa utaratibu mzuri wa kwamba mtu anayeanzisha biashara awe ana miezi Sita kabla ya kuanza kulipa kodi, lakini sasa katika uhalisia *(in practice)* mazingira hayapo hivi. Mpaka sasa bado watu wanatakiwa. Kwa sababu mtu anapoanzisha biashara inabidi kwanza apate leseni ya biashara ili apate leseni ya biashara inabidi aende akapate *TIN* na ili apate *TIN* inabidi apate *TAX Clearance,* sasa ili apate hiyo *TAX Clearance* anapewa makadirio ya kodi na analazimika alipe robo ya kwanza ya yale makadirio ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa analipa kabla hata ya hiyo miezi Sita ambayo amepewa kama muda ambao hatakiwi kulipa kodi. Sasa naomba kujua kwa sababu ni mwongozo na ni utaratibu ambao umetolewa na Serikali lakini kiuhalisia haupo hivyo.

Je, Serikali inatoa majibu gani kuhusiana na changamoto hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri maneno anayosema Mbunge ndiyo uhalisia huo, na mimi ndiyo Jimbo ambalo nimezungukwa na wafanyabiashara, sina wafugaji wala sina wakulima, nina wafanyabiashara na kero ndiyo hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili tulichukue tulifanyie uchunguzi, lakini nitoe maelekezo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kufuata Sheria, Utaratibu na Kanuni zilizowekwa na Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nyakati tofauti Serikali imekuwa ikisisitiza kutokufungia akaunti wafanyabiashara, lakini tumeendelea kupokea malalamiko wafanyabiashara wanafungiwa akaunti. Hata kama kuna changamoto za kikodi lakini kumekuwa na tatizo hilo.

Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa *TRA* kuacha utaratibu wa kufungia akaunti wafanyabiashara hata kunapotokea changamoto za kikodi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba kauli ya Serikali katika jambo hili ni ile kutaka mamlaka ya mapato kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na Serikali katika majukumu yao ya kila siku. Suala la kufunga akaunti bila vielelezo hili hakuna. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendela Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Asha Abdalla Juma

Na. 59

**Hatua kwa Walipakodi Walioshindwa Kulipa**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza: -

Je, ni hatua gani zitachukuliwa kwa walipa kodi walioshindwa kulipa na kuwa na malimbikizo makubwa lakini wapo tayari kulipa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mapato, Sura 438 Kifungu cha 70 na Kanuni zake kinampa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kusamehe adhabu na riba kama kuna suala na sababu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais, Serikali kupitia *TRA* inaendelea kujadiliana na wafanyabiashara wenye malimbikizo ya kodi ili kuwapa unafuu wa kulipa malimbikizo ya kodi kwa awamu bila kuathiri ukwasi, mwenendo na uendeshaji wa biashara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili. Kwanza nashukuru kwa majibu.

Je, ni lini zoezi hili litakamilika ukizingatia umuhimu wa kukusanya kodi na kwa vile ni muda tangu Mheshimiwa Rais alipotoa agizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali na *TRA* ina mkakati gani rafiki wa kufanya makadirio ya kodi kwa wafanyabiashara yanayoendana na mapato halisi ili kuzuia wafanyabiashara wasishindwe kulipa kodi hizi? Ahsante sana,

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali kwanza, inategemea ushirikiano ya mteja wakati wa kufanya majadiliano. Kama mteja atakuwa na ushirikiano mzuri basi suala hili linamalizika kwa kipindi kifupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili; mikakati ambayo tumechukua sisi Serikali ni kutoa fursa kwa wateja, yaani wafanyabiashara, kufanya *self assessment,* yaani

kujifanyia tathmini wenyewe halafu na sisi tunajiridhisha. Mkakati wa pili ni kutoa elimu kwa wafanyabiashara wote ili wafate taratibu za kulipa kodi.

**NAIBU SPIKA:** Asante, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Kyombo kwa niaba Mheshimiwa Kikoyo.

Na. 60

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Omukajunguti**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO K.n.y. MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga uwanja wa ndege wa Omukajunguti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kujenga Kiwanja kipya cha Ndege katika eneo la Omukajunguti, mkoani Kagera ili kuwezesha ndege kubwa ziweze kuruka na kutua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, utekelezaji wa mradi huu utaanza kwa kadri ya upatikanaji wa fedha baada ya Serikali kukamilisha taratibu za utwaaji wa ardhi na ulipaji wa fidia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipatia fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa majibu ya Serikali yenye kutia moyo. Lakini tungependa kujua kutokana na wingi wa abiria katika Mkoa wa Kagera.

Je, ni lini shughuli ya kuwalipa fidia wakazi wa eneo lile kama mchakato wa kuanza ujenzi wa uwanja wa kimataifa wa Omukajunguti itafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokana na wingi wa abiria unaokabili Uwanja wa Ndege wa Bukoba, je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha miruko zaidi ya mmoja ili kukabiliana na mahitaji ya usafiri wa anga kwa wakazi wa Mkoa wa Kagera?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba kuna timu iliundwa na mwezi uliopita ilienda kutembelea eneo la Uwanja wa Omukajunguti ili kujiridhisha kama una uvamizi kiasi gani, ikiwa ni maandalizi ya kuanza kulipa fidia. Kwa hiyo taarifa itakavyotoka taraibu zitaanza ili wananchi waweze kulipwa na maandalizi ya ujenzi wa uwanja huu uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la pili linalohusu miruko, suala la ndege ni biashara pia ni huduma. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Shirika la *Air Tanzania* wamesikia na watafanya tathmini kuona kama kuna umuhimu wa kuongeza safari zingine…

**NAIBU SPIKA:** Ameshakuelewa, ahsante Dkt. Florence.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipatia nafasi.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa upanuzi wa uwanja wa Mkoa wa Kigoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Kibondo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wa Mkoa wa Kigoma kwamba nyaraka za zabuni kwa sasa ziko kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya *vetting* ili kazi ya upanuzi wa uwanja huo zianze. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Asante, Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Ifakara ni mji unaokuwa kwa kasi sana na uwanja wake wa ndege ni dhoofu…

**NAIBU SPIKA:** Swali Mheshimiwa Asenga, acha mikwara.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itakarabati Uwanja wa Ndege wa Ifakara ili ndege kubwa ziweze kutua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asenga Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tulichukue. Hata hivyo niwaagize watu wa *TAA* na *TANROADS* wautembelee uwanja huo kwa ajili ya kuufanyia ukarabati. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar kwa niaba Mheshimiwa Tabasam.

Na. 61

**Ujenzi wa Barabara ya Kahama – Nyangh'wale – Busisi Hadi Sengerema**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya Kahama – Nyangh'wale – Busisi hadi Sengerema itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyangh'wale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi milioni 300 kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kahama – Nyangh'wale – Busisi hadi Sengerema yenye urefu wa kilometa 163. Baada ya kazi hiyo kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa barabara ile inaunganisha na barabara ya Sengerema- Ngoma, je ni lini itafanyiwa usanifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, barabara ya Sengerema- Kamanga imeshafanyiwa usanifu, leo ni miaka mitatu; je, ni lini itajengwa kwa lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tabasam Mbunge wa Sengerema kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Sengerema- Ngoma haijafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na ipo kwenye Ilani. Tumemwagiza meneja wa Mkoa wa Mwanza aweze kuangalia kama kutapatikana fedha yoyote kwenye fedha ya maendeleo basi aielekeze kufanya usanifu wa barabara hii kwa sababu ni barabara fupi sana. Na barabara ya Sengerema – Kamanga Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri, Mheshimiwa Chege, ajiandae Babutale..

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Utegi-Shirati mpaka Kilongwe ni barabara ya kimkakati inayounganisha nchi mbili kati ya Tanzania pamoja na Kenya kwa kupitia Wilaya ya Rorya. Na kwa kuwa tayari upembuzi yakinifu wa barabara hii umeshakamilika nilitaka nijue ni lini sasa barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chege, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ni muhimu kwa sababu inaunganisha Tanzania na Kenya. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Babutale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua barabara yetu ya Ubena Zomozi-Ngerengere ya kilometa 10?

**NAIBU SPIKA:** Hilo ndilo swali la Kibunge, barabara yetu ya Kilometa 10, imekwisha, unaanza sijui tulitoka huku tumekwenda huku! Mheshimiwa Waziri na majibu *short and clear.*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Taletale Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mbena Zomozi imeshapata kibali kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami hizo kilomita alizozisema. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Asante, Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kabula kwa niaba Mheshimiwa Kakoso.

Na. 62

**Ujenzi Wa Bandari Mkoa Wa Mwanza**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO K.n.y. MHE. KABULA E. SHITOBELO** aliuliza: -

Je, ni lini serikali itakamilisha ujenzi wa bandari zilizopo Mkoa wa Mwanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabula Enock Shitobela, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* imekuwa ikiboresha miundombinu ya Bandari za Mwanza Kaskazini na Kusini kwa kutumia bajeti zinazopangwa kila mwaka. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, *TPA* imekamilisha uboreshaji wa jengo la abiria, awamu ya kwanza na matenki manne ya kuhifadhia mafuta katika Bandari ya Mwanza Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka fedha 2022/2023 Serikali kupitia *TPA* imepanga kufanya utanuzi wa eneo la maegesho ya meli *(berth extension),* kuongeza kina cha maji *(dredging)* barabara ya kuingia Bandarini na kuboresha miundombinu saidizi katika bandari ya Mwanza Kaskazini. Kwa upande wa Bandari ya Mwanza Kusini, *TPA* imepanga kuongeza eneo la maegesho ya meli *(berth extension),* barabara ya kuingia Bandarini na uboreshaji wa Miundombinu saidizi. Aidha, uboreshaji huo utaenda sambamba na ununuzi wa mitambo ya kuhudumia mizigo bandarini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imejipanga kupanua bandari za Mwanza na Bandari zile za Nansio; je, Serikali imechukua hatua gani za haraka kuhakikisha wanakamilisha hizo bandari ili ziweze kuwasaidia wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Serikali imekamilisha ujenzi wa Bandari ya Karema na tayari ilishaanza kufanya kazi; je, ni lini Serikali itaanza kuleta meli kwenye eneo la Bandari ya Karema, meli za kimataifa na meli za ndani? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kakoso kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imekuwa ikipanga fedha katika bajeti mbalimbali hususan kupitia *TPA* kwa bandari hizi za Mwanza, Nansio, Mwanza Kusini na Mwanza Kaskazini. Na hivi navyosema Bandari ya Nansio tayari tumeshafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni pamoja a Bandari za Bukoba pamoja na Kemondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusiana na meli za Kwenda kwenye bandari yetu ambayo imezinduliwa hivi karibuni na hususan katika Ziwa Tanganyika, tunataraji hivi karibuni tutafanya mkutano na washirika ambao ni wadau muhimu katika usafirishaji wa bandari za Ziwa Tanganyika kutoka Congo, Zambia, Rwanda na Burundi. Kwa hiyo hivi karibuni utaanza kuona meli zikienda katika bandari hiyo mpya ya Kalema. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Bandari ya Nansio ina hali mbaya na inaweza kuleta matatizo muda wowote, Mheshimiwa Waziri uko tayari baada ya Bunge hili utembelee Jimbo la Ukerewe ili uone umuhimu wa kuharakisha matengenezo ya bandari ile ya Nansio? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nipo tayari mara baada ya Bunge wiki ijayo tutembelee bandari hii ya Nansio na kujionea; na nitaambatana na wataalam ili washauri vizuri zaidi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ningependa kufahamu, ni lini Serikali inatarajia kujenga vituo vya kupumzikia abiria na mageti ya kushushia abiria kwenye vituo vya Kilondo, Lupingu na Manda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, anataka kujua ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ziwa Nyasa tumeshafanya upembuzi yakinifu katika Bandari za Nyasa pamoja na Mbamba Bay. Kwa hiyo katika mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga katika maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Jesca kwa niaba ya Mheshimiwa Kabati.

Na. 63

**Hitaji la shule ya watoto walioathirika na ukatili wa kijinsia- Kikanda**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU** aliuliza: -

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha shule maalum kikanda ili kusaidia watoto walioathirika na ukatili wa kijinsia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwasaidia Watoto manusura wa ukatili, ambapo imeweka mifumo mbalimbali ikiwemo; Kamati za Jamii za Ulinzi wa Wanawake na Watoto; Madawati ya Jinsia kwenye Vituo vya Jeshi la Polisi na Magereza; Vituo vya Mkono kwa Mkono kwenye Hospitali; Madawati ya Jinsia Vyuo Vikuu na Kati; Madawati ya Ulinzi wa Watoto Shule za Msingi na Sekondari; pia Nyumba Salama kwa ajili ya Manusura kupata huduma jumuishi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa ukatili huo upo nchi nzima, kwa nini vituo hivi vimejengwa katika mikoa miwili tu yaani Dodoma vituo 20, Dar es Salaam vituo 10, ilhali changamoto hii ipo nchi nzima ikiwepo Mkoa wetu wa Iringa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara hii sasa haioni haja ya kushirikiana a Wizara ya Elimu ili kuwa na shule maalum zitakazotoa msaada kwa watoto walioathirika na ukatili huo kama ilivyofanyika katika programu ya MEMKWA?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Kabati Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu hivi vituo 30 vilivyoanzishwa vilikuwa ni vituo vya awali vya majaribio ili kutuwezesha kuona jinsi mfumo unavyofanya kazi. Kwa sasa tumeshaona na tayaru tuko kwenye maandalizi ya mwongozo wa jinsi ya kuvianzisha na kuviendesha nchi nzima, katika mikoa yote. Tunatarajia mapema mwakani mwongozo ukamilike ili tuende nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili kuhusu kuufanya mfumo tuwe kama mfumo wa MEMKWA katika suala zima la kuwafundisha hawa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo uliopo unafanya kazi vizuri kiasi kwamba mtoto anapokutwa na matatizo anapata huduma za kisheria, kisaikolojia, kiafya, chakula na tunamrejesha kuendelea na maisha. Ikitokea sasa kuna tatizo lingine linalozuia asiendelee vizuri tunawapeleka kwenye nyumba salama makao ya watoto na hapo tunaungana na Wizara ya Elimu kutafuta aendelee shule gani tofauti na ile ya awali. Hivyo basi, tumepokea maoni kama itabidi iwe hivyo tutajadili na Wizara ya Elimu kwa nyakati zijazo tuone jinsi ya kufanya, lakini sasa hivi mfumo unafanya kazi vizuri, tunaomba...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri amekuelewa, umejibu vizuri sana, ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Chumi.

No. 64

**Kuongeza Uhai wa Pasipoti za Muda za Kusafiria**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kuongeza uhai wa paspoti za muda wanazopewa Madereva hadi kufikia Miezi sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Pasipoti za muda wanazopewa madereva ni hati za dharura za safari *(Emergency Travel Documents)* ambazo kwa mujibu wa Sheria ya Pasipoti na Hati za Safari ya Mwaka 2002, hutolewa kwa safari moja kwa muda ulioainishwa ndani ya hati husika. Aidha, hati hii ya safari hutolewa kwa waombaji wenye safari za dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la kuongeza muda wa hati za dharura za safari litahitaji mabadiliko ya sheria endapo itaridhiwa, Serikali inawashauri madereva kuomba pasipoti ili kuepuka usumbufu wa kuomba hati za dharura za safari mara kwa mara kwa vile safari zao siyo za dharura. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali na kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sekta ya uchukuzi ina mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu na madereva ndio wahusika wakubwa: Je, Serikali haioni umuhimu wa kuleta mabadiliko haya ya sheria ili hili kundi maalum likapata hizo hati za dharura walau kwa muda wa miezi sita hadi mwaka mmoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Kwa kuwa kupata *Passport* ni mchakato unaochukua siku kadhaa; je, Serikali iko tayari kuwa na dawati maalum kwa ajili ya kuwahudumia madereva ambao wako tayari kupata *Passport* za kudumu wapate huduma kwa haraka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili nya nyongeza ya Mheshimiwa Chumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli upo umuhimu wa hawa madereva kuwa na *passport,* lakini kwa sababu mchakato wa kutoa *Passport* kwa maana ya kuongeza muda wa *Passport* za dharura kuzidi mwezi mmoja uliopo sasa unahitaji mchakato wa mabadiliko ya sheria, ni ushauri wetu; kwa sababu hizi safari wanazifanya mara kwa mara, hakuna sababu za kwa nini wasipate hizi *passport.* Akiipata *Passport* kwa miaka 10 watakuwa wanazitumia hizi *passport.* Kwa hiyo, huenda kukawa na nafuu kuliko kupata *Passport* za dharura mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwa sababu ya kujua umuhimu wa madareva na safari zao, Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Idara ya Uhamiaji imeweka dirisha maalum la kuwahudumia madereva hawa ili pindi wafikapo wasikae foleni muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 65

**Programu za Uvunaji Maji ya Mvua**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-**

Je, ni programu zipi zinatekelezwa kuvuna maji ya mvua na asilimia ngapi ya Wananchi hutumia huduma hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilibuni Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP)* inayotekelezwa nchini kote kuanzia mwaka 2006 hadi 2025. Programu hiyo inatekelezwa kupitia Programu ndogo tatu ambapo pamoja na mambo mengine, programu hizo zinazingatia uvunaji maji ya mvua kwa kuelekeza ujenzi wa mabwawa makubwa, ya kati na madogo na pia, uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia programu hizo, mabwawa yamejengwa na kukarabatiwa kwenye maeneo mbalimbali nchini na katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa mabwawa ya ukubwa wa kati na madogo katika wilaya 16, ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Farkwa na Kidunda na usanifu wa ujenzi wa mabwawa katika Wilaya 24. Aidha, Serikali ilitoa mwongozo wa Uvunaji wa Maji ya Mvua kupitia mapaa ya nyumba kwa watu binafsi na taasisi za Umma na kwa sasa miundombinu hiyo inaonekana katika maeneo mbalimbali nchini. Serikali itatafiti kufahamu ukubwa wa matumizi ya teknolojia hiyo nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Je, ni lini sharti litawekwa sasa baada ya kutoa mwongozo huo *(Building Regulations)* ya majengo yote ya Serikali na hata ya watu binafsi kuwa na makingamaji ili waweze kuihifadhi hayo maji ya mvua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Kwa kuwa maji hayo yanaharibu sana barabara wakati wa masika, hasa maeneo ya mlimani kama ya Wilaya zote za Mkoa wa Kilimanjaro na yanaosha kabisa ile changarawe kwenye barabara: Ni lini mitaro mikubwa itajengwa katika barabara hizo ili iwe salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya, lakini kubwa ambalo nataka nimhakikishie kupitia Wizara yetu ya maji tumeshatoa maelekezo na tumekubaliana kwamba mvua isiwe maafa, mvua iwe fursa. Kwa hiyo, moja ya mkakati wetu ni kuwa na ushirikiano na Wizara nyingine, kwa maana ya Wizara ya TAMISEMI. Mwananchi kule anapotaka kujenga nyumba yake, basi uwekwe utaratibu namna gani anaweza kuvuna maji ya mvua ili aweze kuondokana na matatizo ama changamoto ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kikubwa, Wizara ya Maji itashirikiana na Wizara nyingine ikiwemo Wizara ya TAMISEMI ili kuhakikisha wananchi wetu nyumba wanazojenga wanaweka miundombinu ya uvunaji wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine, tumeona baadhi ya maeneo mbalimbali mvua inaponyesha inaleta maafa na kuleta athari mbalimbali. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais katika Wizara yetu ya Maji ni juu ya ujenzi wa mabwawa ili kuhakikisha kwamba tunavuna maji na kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kujenga miundombinu ili mvua zinaponyesha zisilete athari na badala yake iwe fursa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, muda wetu umekwisha. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Kwa niaba ya Mheshimiwa Daniel, Mheshimiwa Zaytun.

Na. 66

**Miundombinu ya Skimu ya Mbuganyekundu**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha miundombinu ya Skimu ya maji katika Kijiji cha Mbuganyekundu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kujenga miundombinu ya umwagiliaji ya skimu zilizopo katika bonde la Eyasi zenye jumla ya hekta 5,000 ikiwemo skimu ya Mbuganyekundu. Taratibu za kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa skimu hizo unaendelea ambapo zabuni zimeshatangazwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Mto wa Ngainanyuki katika Wilaya ya Longido ni muhimu sana kwa kusaidia kilimo cha umwagiliaji: Je, Serikali ina mkakati gani wa kusanifu miundombinu ya mto huu ili kuwasaidia wananchi wa Longido? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika moja ya mikakati ambayo Wizara tunayo ni kuhakikisha ya kwamba tunatumia ipasavyo vyanzo vya maji katika maeneo yote ya mabonde ili tuweze kufanya kilimo cha umwagiliaji. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa hili ambalo limewasilishwa litakuwa ni sehemu ya mipango yetu na tunaielekeza Tume ya Umwagiliaji kuweza kufika na kuliangalia eneo hilo mara moja kwa ajili ya kuendelea na taratibu nyingine.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Soud Mohamed Juma, Mbunge wa Donge.

Na. 67

**Kuboresha *The National Herbarium of Tanzania* – Arusha**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kuboresha *The National Herbarium of Tanzania Arusha* ili kuimarisha huduma za utafiti na uhifadhi wa Mimea nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *The National Herbarium of Tanzania* ilianzishwa kwa Sheria ya *TPRI* ya Mwaka 1979. Ili kuimarisha utendaji wa Taasisi za Wizara, Serikali imeunda Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu *(TPHPA)* iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 04 ya Mwaka 2020 kwa kuunganisha Sehemu ya Afya ya Mimea iliyokuwa chini ya Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki *(TPRI)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha *The National Herbarium of Tanzania* na kuimarisha Huduma za Utafiti na Uhifadhi wa Mimea, Serikali imepanga kuendeleza kuimarisha kanzidata ya mimea ya Tanzania inayohifadhi sampuli kavu ndani ya *National Herbarium of Tanzania (NHT)* pale Arusha, Mweka, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na *TAFORI*. Aidha, Serikali kupitia *TPHPA* inaendelea Kuorodhesha, kukusanya na kutambua sampuli za mimea katika misitu ya hifadhi nne ambazo ni Mlima Hanang, Chenene, Salanga na Chemichemi, katika mikoa ya Manyara na Dodoma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Soud.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza: Kwa kuwa *Herbarium* ya *TPRI,* Arusha ni kituo muhimu cha uhifadhi na utafiti: Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuajiri na kuzalisha wataalam zaidi ili kuweza kukusanya *data* nchi nzima badala ya ku-*concentrate* na mikoa miwili tu hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili: Kwa kuwa wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, hususan misitu, wana utaalamu mkubwa wa usimamizi wa *Herberium:* Kwa nini tusiangalie uwezekano wa kuhamisha usimamizi wa hii *National Herbarium* kuipeleka maliasili au

angalau kuwa-*engage* watu wa Maliasili wakasaidiana ili kuboresha au kuongeza wigo wa uhifadhi, utafiti na utalii katika *herbarium* zetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kuhusu kuajiri, kwa sababu, nimezungumza pale awali kwenye majibu yangu ya msingi kwamba hii tayari imeshahamia ndani ya Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu, ambayo tumeanza kupitia pia muundo wake na hivi sasa tunahakikisha kwamba tunawapatia nafasi pia kuweza kuajiri wataalamu zaidi kwa sababu muundo huu tunaupitia. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba na hilo pia litakuwa ni sehemu kati ya *priorities* kuhakikisha kwamba, tunakuwa na wataalamu wa kutosha katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu kuhamisha, jambo hili lipo kisheria na hivyo linahitaji marekebisho ya sheria, lakini tumepokea kama Serikali hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

Mheshimiwa Waziri Mkuu anaomba Kutoa Taarifa kwa Mheshimiwa Spika kuwa, amemteua Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

Karibu sana Mheshimiwa Mbarawa. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wageni 19 waliopo jukwaa la Spika; kutoka Benki ya *NMB* ambao ni Ndugu Ruth Zaipuna, Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya *NMB;* Ndugu Lilian Kisamba, Meneja wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR); Ndugu Filbert Mponzi, Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara; Ndugu Benedicto Baragoma, Afisa Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani; Ndugu Emmanuel Akonaay, Afisa Mkuu wa Rasilimali Watu; Ndugu Doreen Joseph, Afisa Mkuu wa Tahadhari; Ndugu Oscar Nyirenda, Kaimu Afisa Mkuu wa Udhibiti; na Ndugu Donatus Richard, Meneja Kanda ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Janeth Shango, Meneja Kanda ya Kusini; Ndugu Dismas Propsper, Meneja Kanda ya Kaskazini; Ndugu Naima Shaame, Mkuu wa Biashara Zanzibar (Unguja na Pemba); Ndugu Jonitha Mrengo, Mkuu wa Idara ya Rasilimali Watu; Ndugu Francis Mittah, Mkuu wa Kitengo cha Mpango Mkakati; Ndugu Vicent Mnyanyika, Kaimu Mkuu wa Idara ya Mawasiliano na Uhusiano wa Umma; Ndugu Ramuna Kassim, Meneja Mwandamizi Rasilimali Watu; Ndugu Mercy Nyange, Meneja Masoko, Matukio, Chapa na Udhamini; Ndugu Nsolo Mlozi, Meneja Kanda ya Kati; Ndugu Grace Matemu, Meneja wa Tawi la Bunge. *(Makofi)*

Mkurugenzi Mkuu, hawa wanaopigiwa makofi, ndio tunaishinao sana humu. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Bunge ambao walisoma na Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*LLB; Alumni 1998* - 2001) wakiongozwa na Ndugu Nelly Mwasongwe, Charles Mugila na Elizabeth Kilassa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Bunge ambao ni viongozi wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu Minja Spencer, Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(DARUSO)*. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Wabunge, wasimame kwa pamoja. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wageni 48 ambao ni Watendaji wa Serikali za Mitaa, Wilaya ya Mpwapwa. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 26 kutoka Kanisa la *Moravian Tanzania,* Jimbo la Kusini Magharibi, Ushirika wa Mbeya. Karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba, siku ya Jumapili, Tarehe 18, kutakuwa na Semina kwa Wabunge wote itakayohusu Miradi ya Anuani ya Makazi, Tanzania Kidijitali, Mkono wa Taifa wa Mawasiliano, Maandalizi ya Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali pamoja na masuala ya mtandao. Semina hiyo itaendeshwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia Saa 5.00 asubuhi. Waheshimiwa Wabunge wote mnatakiwa kuhudhuria semina hiyo muhimu.

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba kuwatangazia Wabunge wote; mnakumbushwa kuwa, kama ilivyotangazwa na Mheshimiwa Spika, kesho Jumamosi, tarehe 17 Septemba, 2022 kutakuwa na Bonanza la Michezo kati ya *Bunge Sports Club* na Benki ya *NMB* itakayofanyika katika viwanja cha *Chinangali Park* ambapo michezo mbalimbali itafanyika kama ifuatavyo: Mpira wa Kikapu (wanaume na wanawake), Mpira wa Pete, Mpira wa Wavu (wanaume na wanawake), Mchezo wa Kuvuta Kamba (wanaume na wanawake), Mchezo wa Kukimbiza Kuku na Mpira wa Miguu.

Michezo hiyo, itatanguliwa na matembezi yatakayoanza katika viwanja vya Bunge Saa 12.00 asubuhi na kuishia katika viwanja vya *Chinangali Park* ambapo michezo mingi itafanyika muda wa asubuhi na mchezo wa mpira wa miguu utafanyika kuanzia Saa 9.00 alasiri katika Viwanja vya *Kilimani Club.* Aidha, mara baada ya michezo hiyo, Wabunge wote wanakaribishwa kwenye mchapalo utakaofanyika katika Viwanja vya *Chinangali* kuanzia Saa 1.00 jioni.

Mgeni Rasmi katika bonanza hilo na wakati wa Mchapalo atakuwa ni Mheshimiwa Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote, pamoja na Watumishi wa Ofisi ya Bunge mnakaribishwa kushiriki kikamilifu katika bonanza hilo. Vifaa vya michezo kwa washiriki wote vitaanza kugawiwa leo Ijumaa kuanzia Saa 5.00 asubuhi kwenye Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika alishatoa taarifa kuwa, kutakuwa na maswali mengi na yatachukua muda wa saa moja na nusu. Naomba tu kwa upande wa Serikali, wakati mnajibu maswali, mna *tendency* ile ya kiprotokali ya kusema naomba sasa kujibu swali la Mbunge fulani fulani; sasa maswali yakiwa zaidi ya 20 kwa sekunde tatu tatu tunatumia kama dakika nne za ziada kwa muda wa Kiti.

Mbunge akiuliza swali, je, barabara hii itajengwa Lini?

Jibu pale; barabara hii itajengwa wiki hii au wiki ijayo au mkataba uko hatua gani. Sasa mtakapoanza kuzungukazunguka, mnachukua muda mwingi sana wa Kiti. Nawaomba tu, hili hasa namwomba Waziri wa Fedha kama yupo, *anyway,* hili nitaliacha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.39 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 19 Septemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*